## TANZANIA YAPATA TUZO KIMATAIFA KUPITIA MFUMO WA E-MREJESHO

# eGA yazidi kung'ara katika maendeleo ya TEHAMA

**Na Joyce Kasiki**

**MAMLAKA ya Serikali Mtandao (eGA) ni kati ya Taasisi muhimu zaidi za Serikali ambayo imepewa jukumu la kuratibu na kusimamia matumizi ya teknolojia katika taasisi za umma kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuongeza ufanisi wa kazi serikalini. Mamlaka ya Serikali Mtandao ilianzishwa ili kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika na mabadiliko ya kidigitali yanayotokea duniani ambapo kupitia dira yake ya kuleta serikali ya kidigitali, eGA imefanikiwa kujenga mifumo mbalimbali inayoiwezesha serikali kutoa huduma kwa njia ya kiteknolojia, kwa uwazi, ufanisi na kwa gharama nafuu. Mojawapo ya mifumo hiyo ni mfumo wa e-Mrejesho, ambao sasa umeweka historia kwa kushinda tuzo ya kimataifa. Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa la kidigitali lililobuniwa kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano kati ya wananchi na taasisi za serikali ambapo kupitia mfumo huo, mwananchi anaweza kutoa malalamiko, maoni au mapendekezo na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na taasisi husika kuhusu taarifa alizotoa. Mfumo huo ni suluhisho la kipekee la kidemokrasia linalowapa wananchi sauti na nafasi ya kushiriki moja kwa moja katika uboreshaji wa huduma za umma. Mwananchi anaweza kutumia mfumo huu kwa kupiga *152*00# kisha kuchagua namba 8 na kisha 2, pia kwa kutembelea tovuti ya www.e-mrejesho.gov.go.tz, au kwa kupakua programu ya e-Mrejesho kwenye simu yake ya mkononi. Njia hizi zimebuniwa kwa kuzingatia uwezo na hali halisi ya Watanzania wengi, na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma kwa urahisi zaidi.**




Meneja Mawasiliano wa eGA, Subira Kaswaga, anazungumza hivi karibuni katika maonyesho ya 49 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, ambapo anasema ,mfumo wa e-Mrejesho umeongeza uwazi na uwajibikaji katika taasisi za serikali, na kuchangia kwa kiasi kikubwa kujenga imani ya wananchi kwa serikali yao.

"Mfumo huu si tu kwamba unamrahisishia mwananchi kufikisha kero zake, bali pia unaweka taasisi kwenye muktadha wa kuwajibika haraka na kwa uwazi," anasema Kaswaga.

Anasema jitihada hizo za eGA zimetambulika kimataifa pale ambapo Tanzania, kupitia mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (e-Mrejesho V2), ilitangazwa mshindi katika kipengele cha Serikali Mtandao kwenye Tuzo za Mkutano wa Dunia

wa Tukio la Ngazi ya Juu la Jukwaa la WSIS+20 (WSIS+20 Forum High-Level Event), uliofanyika mjini Geneva USWIS kuanzia Julai 7 hadi 11 mwaka huu ambapo Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari alipokea tuzo hiyo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Tuzo hizo ambazo huratibiwa na Shirika la Mawasiliano la Umoja wa Mataifa (International Telecommunications Union – ITU) zinalenga kutambua na kuchochea miradi bunifu, inayotumia TEHAMA katika kuchangia maendeleo endelevu duniani.

Kaswaga amesema, Mfumo wa e-Mrejesho toleo la pili (V2), umeibuka mshindi wa tuzo hiyo katika kipengele cha Serikali Mtandao (e-Government AL C7), kati ya mifumo 360 ya TEHAMA iliyofuzu hatua ya awali ya mchujo kutoka kwa zaidi ya maombi 1,000 ya mifumo ya kidijitali yaliyowasilishwa kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Kwa mujibu wa Kaswaga,baada ya mchujo wa awali, mfumo wa eMrejesho ulifanikiwa kuingia kundi la tano bora kupitia taarifa iliyopokelewa na e-GA kutoka ITU kwa njia ya baruapepe.

Mfumo wa e-Mrejesho (V2) umesanifiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), ukiwa umeboreshwa kwa kutumia teknolojia ya Akili Mnemba (Artificial Intelligence – AI) katika kukusanya maoni ya wananchi.

Kaswaga anasema,ushindi huo ni ishara kuwa Tanzania inatambulika duniani kama nchi inayoweza kubuni na kutumia teknolojia kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Aidha akatumia nafasi hiyo kuhamasisha wananchi kuendelea kutumia mfumo huo kwani unaonyesha namna serikali ilivyo tayari kupokea mrejesho wa moja kwa moja kutoka kwa wananchi na kuufanyia kazi huku akizihimiza taasisi zote za umma kutumia kikamilifu mfumo huo ili kushughulikia changamoto na kuongeza ufanisi wa huduma.

Mbali na e-Mrejesho anasema , eGA imefanikiwa kujenga mifumo mingine yenye mchango mkubwa katika kupunguza urasimu na kuleta huduma karibu zaidi na wananchi.

Anasema,Mojawapo ya mifumo hiyo ni M-Gov (Huduma za Serikali Kupitia Simu za Mkononi), ambao huruhusu wananchi kupata huduma mbalimbali kwa kutumia simu za kawaida ,mfumo huu hauhitaji intaneti na hauna gharama kwa mtumiaji, jambo linaloufanya kufikiwa hata na wale wasio na simu janja.

Kwa mujibu wa Kaswaga ,kupitia M-Gov, wananchi wanaweza kulipia huduma mbalimbali kama umeme, maji, leseni, na nyinginezo kwa urahisi na haraka ambalo ni suluhisho madhubuti kwa nchi kama Tanzania, ambako idadi kubwa ya wananchi bado wanatumia simu za kawaida.

Vile vile anasema,eGA imeanzisha mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini, ambao unaziwezesha taasisi za umma kushirikiana na kubadilishana taarifa kwa njia ya kidigitali ili kurahisisha utendaji kazi na kutoa huduma bila ya mwananchi kulazimika kuhangaika kutoka ofisi moja hadi nyingine.

" Kwa mfano, kama mwananchi anahitaji huduma ya NIDA inayohusisha taarifa kutoka TRA, kupitia mfumo huu taasisi hizo zinaweza kuwasiliana moja kwa moja bila mwananchi kuzunguka kutoka ofisi moja kwenda nyingine."anasema

Katika kuhakikisha usalama wa taarifa na mifumo ya serikali, eGA pia imebuni mfumo wa uthibitisho wa mara mbili (multi-factor authentication). Mfumo huu unahitaji mtumiaji kuthibitisha utambulisho wake kwa njia ya pili, kama vile ujumbe kwenye simu, kabla ya kupata huduma au kuingia kwenye akaunti,hii ni hatua muhimu ya kulinda taarifa binafsi za watumishi na taarifa nyeti za serikali.

Mafanikio haya yote hayawezi kupatikana bila uwekezaji katika utafiti na ubunifu. Kwa kuliona hilo anasema, eGA imeanzisha Kituo cha Utafiti na Ubunifu wa Serikali Mtandao, ambacho hutoa fursa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, watafiti na wabunifu wa TEHAMA kushirikiana katika kuunda suluhisho za kiteknolojia. Kituo hiki hutoa mafunzo kwa vitendo, nafasi za kujitolea, na mazingira rafiki kwa wabunifu chipukizi kufanya kazi zao.

Anasema,kwa kushirikiana na taasisi za elimu ya juu, kituo hiki kinaibua vipaji vipya, kuendeleza tafiti zenye tija na kuleta mifumo bora inayokidhi mahitaji ya serikali ya kisasa. Hii ni njia ya kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na wataalamu wa ndani wenye uwezo wa kushindana kimataifa.

Kaswaga anasisitiza kuwa teknolojia inabadilika kwa kasi, na ni lazima Tanzania iwe tayari kwenda sambamba na mabadiliko hayo ambapo ansema "Hatuwezi kusubiri,ndiyo maana tumebuni kituo hiki , ni jukwaa la kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa sehemu ya mabadiliko ya dunia kupitia TEHAMA,"

Kwa ujumla, mafanikio ya eGA si ya kupuuzia. Kutambulika kimataifa kupitia mfumo wa e-Mrejesho ni ishara ya mwelekeo sahihi.

